



KUJINYENYEKEZA – MBINU ZA MAPAMBANO YA KUJIHAMU

*Yakobo 4:7 "Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia."*

FANYA SEHEMU HII YA KWANZA KILA SIKU

**1. Kila siku mtii Mungu.**

Maombi ya Kujinyenyekeza. “Baba wa Mbinguni, ninakupa wewe umiliki wa ufahamu, hisia, ridhaa na mwili wangu. Ninakualika uwe Bwana wa maisha yangu, katika Jina la Bwana Yesu Kristo.”

**2. Vaa silaha za Mungu.**

Maombi ili kuvala silaha za Mungu. “Bwana, ninazivaa silaha zako uliz-onipa: Mkanda wa Kweli (Kujifunga Kweli kiunoni), Diri ya haki, maandalizi ya Injili ya Amani, ngao ya imani, chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho” (Waefeso 6:10-18).

**3. Mfunge Shetani.**

Maelezo ya Kufunga na Kufungua. “Shetani, ninakufunga. Hutakuwa na uwezo wa kutawala akili, hisia, ridhaa au mwili wangu. Ninajifunga mwenyewe kutoka kila ngome na vifungo vyote katika Jina la Bwana yesu Kristo”.

**4. Kama umetoa nafasi kwa adui, jinyenyekeze na kukiri dhambi na kisha zipinge na kuzikemea na kiziamuru zitoke roho zilizokushambulia.**

Maombi ya Kukiri.

“Baba, ninakuja kwako katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Nimetoa nafasi kwa roho za \_\_\_\_\_. Hazitoki kwako na wala sizitaki katika maisha yangu. Ninakiri dhambi nilizotenda katika eneo hili la maisha yangu. Nisamehe kwa kuziruhusu roho hizi kuyatawala maisha yangu. Asante kwa kunisamehe, katika Jina la Bwana Yesu Kristo”.

**5. Zungumza/onge hili na adui katika kujihami na kukemea.**

Tamko. “Roho za \_\_\_\_\_ ninachukua mamlaka dhidi yako katika Jina la Yesu Kristo. Nimejisalimisha/nyenyekeza kwa Mungu na huwezi kukaa. Huwezi kuzipata akili au mwili wangu. Ninachukua tena kila eneo ambalo nilikupa wewe katika maisha yangu. Ninajifunga mwenyewe kutoka vifungo vya \_\_\_\_\_. Ninakumuru katika Jina la Bwana Yesu Kristo kuondoka sasa. Ninakumera na kukuamuru kwenda kwenye shimo la kuzimu sasa hivi katika Jina la Bwana Yesu Kristo”.

**6. Ombo na umwalike Roho Mtakatifu kutawala maeneo yote ya mai-sha yako.**

Maombi ya Utakaso. “Baba wa Mbinguni, nakuomba unijaze na kutawala kila eneo liliosafishwa/takaswa katika maisha yangu kwa Roho wako Mtakatifu katika Jina la Bwana Yesu Kristo”.